Ambacho Imani Inahitaji

(What Faith Demands)

Na

Ellis P. Forsman

Ambacho Imani Inahitaji

(What Faith Demands)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Ambacho Imani Inahitaji

Heb. 11:1-6

Imanni inatafsiriwa.

Heb. 11:1-6, "*Basi imani ni kuwa na hakika na mambo ya tarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa. Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri. Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo ijapokuwa amekufa, angali akinena. Kwa imani Henoko alihamishwa asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alishuhudiwa kwamba amempendeza Mungu. Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu, lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Imani huja vipi?

Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Imani inakuwa kamilifu lini?

Yak. 2:22-23, "*Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, nay a kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu.*"

Aina na viwango vya imani

Kuna imani moja. Efe. 4:4-5, "*Mwili mmoja na roho mmoja kama, na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja.*"

Imani kuu. Mat. 8:5-10, "*Hata alipoingia Kapernaumu, akida mmoja alimjia, akamsihi, akisema, Bwana mtumishi wangu amelala nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana. Yesu akamwambia nitakuja nimponye. Yule akida akamjibu, akasema Bwana mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu na mtumishi wangu atapona. Kwa maana mimi nami ni mtu*

niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu nenda, huenda, na huyu njoo, huja; na mtumwa wangu fanya hivi hufanya. Yesu aliposikia hayo alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, amin, nawaambieni, sijaona imani kubwa namna hii, kwa yeyote katika Israeli."

Imani ndogo. Mat. 6:25-30, "*Kwa sababu hiyo nawaambieni msisumbukie maisha yenu, mle nini, au mnywe nini; wala miili yenu mvae nini. Maisha je si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani ya kwamba hawapandi wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je si bora kupita hao? Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua anaweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Na mavazi ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo hayafanyi kazi, wala hayasokoti nami nawaambia ya kwamba, hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama moja wapo la hayo. Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, je hatazidisha sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?*"

Imani dhaifu. Rum. 14:1, "*Yeye aliye dhaifu wa imani mkaribisheni, walakini msimhukumu mawazo yake.*"

Imani yenye nguvu. Rum. 4:17-20, "(ya Ibrahimu), "*(Kama ilivyoandikwa, nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi); mbele zake yeye aliyemwamini, yaani, Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako. Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa ndivyo utakavyokuwa uzao wako. Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu.*"

Imani inahitaji mambo matatu

Kukubali na kumtii Mungu na neno lake.

Matendo (ama unaweza kuona sababu ya Mungu , au hapana).

Hakuna mkato katika mpango wa Mungu.

Mifano ya haya:

Nuhu. Heb. 11:7, "*Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo*

akauhukumu ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani."

Ibrahimu.

- Heb. 11:8-10, "*Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye katika ahadi ile ile. Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao wenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.*"

- Heb. 11:17-19, "*Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye aliyezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee; naam, yeye aliyeambiwa, katika Isaka uzao wako utaitwa, akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano.*"

- Yak. 2:21-24, "*Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu. Mwaona kwamba Mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani pekee yake.*"

Yoshua (ukuta wa Yeriko). Heb. 11:30, "*Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba."*

Uongofu wa Sauli wa Tariso.

- Mdo. 9:3-9, "*Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafla ikamwangaza kotekote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi? Akasema U nani wewe Bwana? Naye akasema mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe. Lakini simama uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda. Na wale watu waliosafiri pamoja naye wakasimama kimya, wakiisikia sauti wasione mtu. Sauli akainuka katika nchi, na macho yake yalipofumbuka, hakuona kitu; wakamshika mkono wakamleta mpaka Dameski. Akawa siku tatu haoni; hali, wala hanywi.*"

- Mdo. 22:11-16, "*Na nilipokuwa sioni kwa sababu ya fahari ya nuru ile, nikaongozwa na mikono yao waliokuwa pamoja nami nikaingia Dameski. Basi mtu mmoja Anania, mtauwa kwa*

kuifuata sheria, aliyeshuhuddiwa wema na Wayahudi wote waliokaa huko, akanijia akasimama karibu nami, akaniambia ndugu yangu Sauli, uone. Nikamwinulia macho yangu saa ile ile. Akasema Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake, na kumwona yule mwenye haki, na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake. Kwa maana utakuwa shahidi wake kwa watu wote, wa mambo hayo uliyoyaona na kuyasikia. Basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake."

Matumizi kwetu (kutumia vitu katika sehemu hiyo hapo juu)

Mpango wa wokovu.

- Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*"
- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Ibada.

- Yoh. 4:24, "*Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"
- Mdo. 20:7, "*Hata siku ya kwanza ya juma tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafululiza maneno yake hata usiku wa manane.*"
- Efe. 5:19, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;*"

Utafuteni kwanza ufalme.

Mat. 6:33, "*Basi utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Kuishi kwa haki.

- Tito 2:11-12, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na*

tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa;"

- Rum. 1:17, "*Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Kushindwa kufanya maelezo haya yote inaonyesha ukosefu wa imani, au udhaifu wa imani.

1 Kor. 4:2, "*Hapo tena <u>inayohitajiwa</u> katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.*"

Hitimisho

Je una imani kufanyaa mapenzi ya Mungu leo na umuamini kwa ajili ya ahadi. Kufanya hivyo mtu anapaswa kufanyika Mkristo. Zifuatazo ni hatua mhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend 11:18, "*...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima.</u>*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu

amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza." Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo?